TANGAZO LA SERIKALI Na. 489 la tarehe. 14/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa au madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mhudumu" maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kampuni, kikundi cha watu au shirika lililoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazototozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa madini ya ujenzi

6. Mtu hataruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayaruhusiwi machimbo ya madini ya ujenzi isipokuwa kama mtu huyo-

(a) amepata kibali cha kufanya hivyo, ambacho kitatolewa na Halmashauri baada ya kulipa ada kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Kwanza;
(b) ametoa taarifa ya kuchimba madini ya ujenzi katika Mamlaka ya Kijiji husika; au
(c) hadaiwi fedha yoyote ambayo inastahili kulipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Ada za kukodi mali za Halmashauri

7. Halmashauri inaweza kukodisha mali zake ikiwemo ukumbi, majengo pamoja na samani mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sehemu B.

Ada ya ukaguzi wa afya

8.-(1) Mtu hataendesha biashara au kutoa huduma ya nyumba ya kulala wageni, hoteli, mgahawa, bucha la kuuza nyama, kilabu cha pombe au baa, bila ya wahudumu wake kupimwa afya.

(2) Huduma za kupimwa afya zitatolewa na Halmashauri kupitia maafisa wake wa afya na kila mhudumu atapaswa kupimwa kila baada ya kipindi cha miezi sita.

(3) Ada itakayotozwa kwa kila mhudumu kupimwa afya itakuwa katika kiwango kilichoainishwa katika Sehemu C ya Jedwali la Kwanza.

Ada ya vibali vya ujenzi

9.-(1) Mtu hataruhusiwa kujenga, kukarabati au kuendeleza kwa namna yoyote kiwanja katika eneo lililopimwa au lililotangazwa kuwa eneo la mipangomiji bila kupata kibali cha ujenzi kilichotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali cha ujenzi yataambatana na michoro au ramani ya jengo iliyoidhinishwa na kwa mujibu wa taratibu ambazo zitaelekezwa na Afisa Mwidhiniwa.

(3) Ada ya kibali cha ujenzi itatozwa kwa kuzingatia utaratibu na viwango vilivyoainishwa katika Sehemu D ya Jedwali la Kwanza.

Muda na namna ya kulipa ada na ushuru

10.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo yote yatafanywa kwa Afisa Mwidhiniwa, benki au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kwa ajili hiyo.

(5) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatatolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia muda wa saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Uteuzi wa Wakala

12.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kukusanya ada na ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atawajibika kukusanya ada na ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(3) Wakala aliyeteuliwa atawajibika kuzingatia masharti na maelekezo katika Sheria Ndogo hii pamoja na sheria nyingine yoyote husika.

Ukusanyaji wa madeni

13.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Makosa

14. Mtu anatenda kosa ikiwa-

(a) anakataa au anashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Mwidhiniwa;
(b) anakataa au anajaribu kukataa kulipa ada na ushuru anaopaswa kulipa;
(c) anamshawishi mtu yeyote, taasisi au kundi la watu kutolipa ushuru; au
(d) anamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu.

15. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa

17. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka, 2013 na

TS Na.178 la 2013 na 174 la 2013

Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru wa Huduma za Ardhi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka, 2013 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

SEHEMU A

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | AINA YA MADINI YA UJENZI | UZITO WA GARI | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchanga | Chini ya Tani 7 | Tshs. 3,000/= kwa tripu |
| | | Tani 7 hadi 10 | Tshs. 4,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 10 hadi15 | Tshs. 5,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 15 hadi 20 | Tshs.10,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 20 | Tshs.20,000/= kwa tripu |
| 2. | Mawe | Chini ya Tani 7 | Tshs. 4,000/= kwa tripu |
| | | Tani 7 hadi 10 | Tshs. 5,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 10 hadi 15 | Tshs. 6,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 15 hadi 20 | Tshs. 15,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 20 | Tshs. 25,000/= kwa tripu |
| 3. | Kifusi | Chini ya Tani 7 | Tshs. 2,000/= kwa tripu |
| | | Tani 7 hadi 10 | Tshs. 3,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 10 hadi 15 | Tshs. 4,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 15 hadi 20 | Tshs. 6,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 20 | Tshs. 10,000/= kwa tripu |
| 4. | Udongo | Chini ya Tani 7 | Tshs. 1,000/= kwa tripu |
| | | Tani 7 hadi 10 | Tshs. 2,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 10 hadi 15 | Tshs. 3,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 15 hadi 20 | Tshs. 5,000/= kwa tripu |
| | | Zaidi ya Tani 20 | Tshs. 10,000/= kwa tripu |
| 5 | Kokoto | Kwa kila mita ya ujazo (meter cubic) | Tshs. 5,000/= |

SEHEMU B
ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| NA | MATUMIZI | KIWANGO CHA USHURU) |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi Ukumbi wa Halmashauri | Tshs. 200,000/= kwa siku |
| 2. | Kodi ya Pango katika majengo ya Halmashauri kwa ajili ya Ofisi | Tshs. 4,000/= kwa kila Mita Moja ya Mraba kwa Mwezi |
| 3. | Kukodi viti | Tshs. 300/= kwa siku |
| 4. | Kukodi Meza | Tshs. 500/= kwa siku |

SEHEMU C
ADA YA UPIMAJI WA AFYA

| NA. | AINA YA SHUGHULI | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Kupimwa Afya kwa Wahudumu wa Nyumba za Kulala Wageni, Hoteli, Migahawa, wauzaji wa Bucha za Nyama | Tshs.5,000/=kwa kila mmoja kila baada ya Miezi Sita |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Kupimwa Afya kwa Wahudumu wa Baa na Vilabu vya Pombe | Tshs.5,000/= kwa kila mmoja kila baada ya Miezi Sita |

SEHEMU D

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| NA. | AINA YA UJENZI | KIASI CHA ADA NA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mnara wa Mawasiliano | Tshs.500,000/= |
| 2. | Kituo cha Mafuta | Tshs.250,000/= |
| 3. | Majengo ya Biashara (Masoko, Hoteli, Baa) | Tshs.100,000/= |
| 4. | Jengo la Ghorofa 1-2 | Tshs.100,000/= |
| 5. | Jengo la Ghorofa 3 na kuendelea | Tshs.200,000/= |
| 6. | Majengo ya Huduma (Shule, Zahanati, Kituo cha Afya) | Tshs.80,000/= |
| 7. | Majengo ya kutolea huduma za Dini (Msikiti au Kanisa) | Tshs.20,000/= |
| 8. | Nyumba za makazi na biashara | Tshs.50,000/= |
| 9. | Nyumba za makazi | Tshs.40,000/= |
| 10. | Ada ya Uzio wa muda (@$M^2$) | Tshs.2,000/= |
| 11. | Maghala ya kuhifadhia (godauni) | Tshs.50,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kondoa, kwamba mnamo tarehe …........… ya mwezi …...…. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …...................… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024. Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……...............…….ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

**MBELE YANGU :**
Jina:…………………………………..……………………….....
Saini………………………..……………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa uliofanyika tarehe 28/4/2022 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHABANI KAPALA MILLAO,
*Mkurugenzi Mtendaji (w),*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

ABDALLAH SALUM MAGUO,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi*